# MASWALI YA KUJIPIMA

Angalia ndani ya kijitabu kwa majibu.

1. Chini ya Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti VVU/UKIMWI, daktari hawezi kuiambia familia yako au marafiki zako kuhusu hali yako ya VVU.
   a) KWELI
   b) SI KWELI

2. Chini ya Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti VVU/UKIMWI, ni halali kwa mwenye nyumba kukufukuza wewe kwa kuwa unaishi na VVU.
   a) KWELI
   b) SI KWELI

3. Unyanyasaji wa kijinsia ni:
   a) Unyanyasaji wa kimwili
   b) Udhalilishaji wa kimapenzi
   c) Unyanyasaji wa kifikra ikiwa ni pamoja na vitisho
   d) Vitendo vyote hapo juu

4. Wanawake wana haki ya kuwa huru kutokana na:
   a) Ugumu wa maisha
   b) Vurugu/vipigo
   c) Huzuni
   d) Ubaguzi
   e) b na d

5. Sheria za Tanzania zinatambua haki za wanawake:
   a) Kumiliki ardhi
   b) Kushikilia au kumiliki hati za ardhi
   c) Kurithi ardhi
   d) a na b
   e) Hakuna kabisa

6. Chini ya sheria za kimataifa, haki ya mwanamke kwenye ardhi ni:
   a) Ndogo au ipo chini zaidi ya ile ya mume wake
   b) Sawa kama wanaume wote isipokuwa pale inapomuhusu mwanandoa mwenzake
   c) Sawa kama wanaume
   d) Inategemea nchi anayoishi

**MAJIBU:**

1. a/ 2. b/ 3. d/ 4. e/ 5. d/ 6. c

# WAPI NAWEZA KUPATA MSAADA?

**ARUSHA**:

**Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake na Haki za Binadamu Arusha (AWLAHURIC)**
Martha Lyimo, Mratibu
CCM Mkoa, Makongoro Road
3rd Floor, Room 14, Arusha
**T: +255 75 4580756 / +255 78 2175325**

**Chama cha Wanawake Wanasheria Tanzania (TAWLA)**
CCM MKOA, 2nd Floor, Room 3
PO Box 996, Arusha
**T: 027 2545154** / info@tawla.or.tz

**DAR ES SALAAM**:

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG)**
Legal Access Advocates
PO Box 2643, Dar es Salaam
**chragg@chragg.go.tz / www.chragg.go.tz**
**T: +255 22 2135747/8** / info@tawla.or.tz

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**
PO Box 75254, Dar es Salaam
**T: +255 22 2773038/48**
www.humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria Tanzania (NOLA)**
P.O. Box 10096, Dar es Salaam
**T: 0744 043006** / msaadawasheria@hayoo.co.uk

**Chama cha Wanasheria Tanzania**
Plot 299, Ruhinde Street, Ada Estate
PO Box 2148, Dar es Salaam
**T: +255 22 2664254** / info@tls.or.tz / www.tls.or.tz

**Chama cha Wanawake Wanasheria Tanzania (TAWLA)**
TAWLA House, Plot 33
Ilala Sharif Shamba
PO Box 9460, Dar es Salaam
**T: +255 (0) 222 862865 / +255 (0) 732 929650**
info@tawla.or.tz

**Women's Legal Aid Centre (WLAC)**
PO Box 79212, Dar es Salaam
**T: +255 22 2664051**

# WANAWAKE

# & SHERIA

# ZIJUE

# HAKI

# ZAKO!

# UNYANYASAJI WA KIJINSIA

**KILA MWANAMKE ANA HAKI YA**:

- KUISHI KWA USAWA & KULINDWA NA SHERIA
- KUWA NA HADHI KATIKA JAMII
- KUWA HURU KUTOKANA NA AINA ZOTE ZA VURUGU, UNYANYASAJI AU UKANDAMIZAJI WA KIMWILI, KIFIKRA, KIJINSIA & KISAIKOLOJIA
- KUWA HURU KUTOKANA NA UBAGUZI WA KIJINSIA

**SHERIA**:

- ***Katiba ya Tanzania:***
  - "Watu wote wamezaliwa huru, na wote ni sawa... Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wana haki ya kupata ulinzi na usawa mbele ya sheria."
- ***Sheria Maalumu ya Makosa ya Ngono – SOSPA (Tanzania)***
- *Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake wa Afrika* ***(Mkataba wa Umoja wa Africa)***:
  - "Kila mwanamke ana haki ya msingi ya kuheshimiwa ambayo kila mwanadamu anazaliwa nayo…"
- ***CEDAW – Mkataba kuhusu kuondolewa kwa namna zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (Mkataba wa Kimataifa)***:
  - "Mataifa Wanachama katika Mkataba huu wana jukumu la kulaani ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake…"

# ARDHI

**KILA MWANAMKE ANA HAKI YA**:

- KUMILIKI ARDHI
- KUNUNUA, KUUZA & KUHAMISHA ARDHI
- KUWEKA JINA LAKE KATIKA HATI YA ARDHI

**SHERIA**:

- ***Katiba ya Tanzania***:
  - Kila mtu ana haki ya kumiliki mali.
  - Ubaguzi wa kijinsia ni umekatazwa.
- ***Sheria ya Ardhi ya Tanzania ya mwaka 1999***: Mwanamke ana haki ya:
  - "kupata, kushikilia na kutumia ardhi."
  - kushirikiana na mume wake katika umiliki wa ardhi, hata kama kuna mke zaidi ya mmoja.
- ***CEDAW***

**URITHI**

**Q:** Je, kuna sheria zenye kulinda haki za wanawake za kurithi?

**A: *NDIYO.*** *Hata hivyo, ukweli ni kwamba sheria ya urithi Tanzania ina ubaguzi dhidi ya wanawake wengi, na zinapingana na sheria nyingine zinazomlinda mwanamke.*

- Wanawake wana haki maalumu ya kurithi mali chini ya sheria ya kikanda.
  - ***Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake wa Afrika***
- Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa mwanamke ana haki sawa kwa kama ile ya mwanandoa mwenzake.
  - ***CEDAW***

# VVU/UKIMWI

**KILA MWANAMKE ANA HAKI YA**:

- KUWA HURU KUTOKANA NA UNYANYAPAA & UBAGUZI KWA MISINGI YA VVU / UKIMWI
- KUIFANYA AU KUIWEKA HALI YAKE YA VVU KAMA SIRI
- KUMILIKI ARDHI HATA KAMA YEYE ANAISHI NA VVU / UKIMWI
- KUWA HURU KUTOKANA UNYAYASAJI WA KIJINSIA HATA KAMA ANAISHI VVU / UKIMWI

**SHERIA**:

- ***Sheria ya kuzuia na kudhibiti VVU/UKIMWI (Tanzania)***

## WAPI NAWEZA KUPATA MSAADA?

**MOROGORO**:
**Morogoro Paralegal Centre**
Flora Masoy, Coordinator
PO Box 6584
Morogoro
**T: 0754 477 928**
moroparalegal@yahoo.com

**DODOMA**:
**Chama cha Wanawake Wanasheria Tanzania (TAWLA)**
NSSF Building
3rd Floor, Room 49
PO Box 1920, Dodoma
**T: (026) 2321484 / (0766) 055763**
info@tawla.or.tz

**TANGA**:
**Chama cha Wanawake Wanasheria Tanzania (TAWLA)**
**T: (097) 2645096**
info@tawla.or.tz